**Zakayo Kusekwa Mbuti, (1928–1999)**

Zakayo Kusekwa Mbuti alikuwa mchungaji wa mstari wa mbele, mkurugenzi wa uchapaji wa fildi, na mkurugenzi wa uchapishaji wa Misheni ya Union Tanzania.

**Kuzaliwa na Familia**

Zakayo Kusekwa Mbuti alizaliwa Julai 15, 1928, katika kijiji cha Nasa- Ihojo, Magu-Mwanza, na kufariki Julai 18, 1999, akiwa na umri wa miaka 71. Baba yake alikuwa Mbuti Ntogwashenji na mama yake alikuwa Milembe Bushmbe. Alikuwa mzaliwa wa pili kati ya ndugu wanane. Wengine walikuwa Malunja, Kubunga, Manota, Buya, Maleba, Mudo, na Ntuji. Alizaliwa katika kabila kubwa zaidi nchini Tanzania, Wasukuma, ambalo linajumuisha takriban asilimia 16 ya watu wote wa nchi hiyo.

Kusekwa alifunga ndoa na Elizabeth Manugwa ambaye alifariki mapema katika ndoa yao na kumuacha na watoto wadogo. Baadaye, katika miaka ya 1970, alimuoa Tezira Nkondo. Mungu aliwabariki na watoto kumi kwa jumla: George, Rebecca, Dorcas, Elizabeth, Mesha, Ngole, Mbuti, Milembe, Salyungu, na Robert.

**Elimu**

Mchungaji Kusekwa alisoma Shule ya Msingi Nyambitilwa wilayani Bunda kuanzia Oktoba 1942 hadi 1946. Walimu wake wa kwanza walikuwa Samson Shuli na Petro Masenge. Mnamo Oktoba 1946, alikwenda Shule ya Kati ya Ikizu ambako alihitimu mwaka 1951. Akiwa anasoma huko alibatizwa na Mchungaji Joram Kamwendo kutoka Malawi. Mnamo 1952 alihudhuria Chuo cha Mafunzo ya Ualimu cha Ikizu . Mnamo Oktoba 7, 1953, Mchungaji Kusekwa alihitimu kama mwalimu aliyehitimu pamoja na wahitimu wengine, akiwemo Mchungaji Elisha Okeyo. Mnamo 1960 Mchungaji Kusekwa alichukua kozi ya huduma ya kichungaji kutoka Chuo cha Waadventista cha Bugema, Uganda. Mwaka 1966 alihudhuria Chuo Kikuu cha Solusi nchini Zimbabwe.

**Mwalimu na Mwinjilisti mwenye Shauku**

Mnamo Februari 7, 1954, Mchungaji Kusekwa alianza kufanya kazi kama mwalimu-mwinjilisti katika shule ya kanisa ya Lagangabilili wilayani Bariadi. Aliwahamasisha watu na waumini wa kanisa hilo kujenga shule na kanisa lililoezekwa kwa mabati. Kazi hii ilifanywa kwa hiari na watu. Tarehe 2 Februari 1959, Mchungaji Kusekwa alijitosa katika mji wa Mwanza na kufungua matawi kadhaa ya Shule za Sabato. Matawi hayo ni pamoja na Gereza la Butimba, Mwanza-Kusini, Nyegezi, Mahina, Igogo, Mabatini, Airport, Kayenze, Bwiru, Butimba TTC, Kisesa, na mengine mengi. Mwenzake katika misheni hii alikuwa Mchungaji Godson Elieneza.

**Awekwa wakfu**

Tarehe 8 Julai 1963, Mchungaji Kusekwa alitawazwa kwa kuwekewa mikono ya mhudumu wa injili. Ibada ya kuwekwa wakfu iliendeshwa na Mchungaji Robert

Pearson, mwenyekiti wa Kitengo cha Trans-Africa. Mchungaji Kusekwa alikuwa mzungumzaji na mwinjilisti mahiri kwa waumini na wasio waumini. Ifuatayo ni baadhi ya mikutano ya injili aliyoshiriki.

**Uinjilisti wa Majiji**

Alihusika kama mshiriki wa timu katika uinjilisti wa jiji ulioendeshwa na wainjilisti wawili mashuhuri—Mchungaji Fares Muganda mwaka wa 1961 na Mchungaji Earl Cleveland mwaka wa 1963. Huyu ndiye aliyeanzisha Kanisa la Waadventista wa Sabato Magomeni jijini Dar es Salaam.

Mwaka 1981 Mchungaji Kusekwa alifanya kazi katika mji wa Bariadi, ambapo juhudi zake zilileta mwanga ndani ya mioyo ya wasikilizaji wake na wengi wakasalimisha maisha yao kwa Kristo.

Mwaka 1989 Mchungaji Kusekwa alihubiri katika mji wa Tarime, ambapo roho 2,500 zilivutwa kwa Kristo, huku 400 kati yao zikitoka katika asili ya Kanisa Katoliki. Dk Daniel Fariji Mtango (mkurugenzi wa huduma ya afya wa Union ya Tanzania) akishuhudia nguvu kubwa ya kuhubiri injili, alisema, baada ya mzee mmoja wa kanisa la Kilutheri kubatizwa, alileta watu wengine kumi pamoja naye ili wabatizwe.

Kuanzia Mei hadi Juni 1990, Mchungaji Kusekwa alihubiri Shinyanga mjini. Zaidi ya watu 1,000 walibatizwa. Dk. Robert Taylor (Mwenyekiti wa Misheni ya Union ya Tanzania) alitoa Biblia 1,500 na seti 1,500 za masomo ya Biblia. Chini ya uongozi wa Joseph Bohole, karibu watu 2,121 walihusika katika kujifunza Biblia. Kwa sababu hiyo, zaidi ya nusu yao walibatizwa.

Mnamo Julai 1992 katika mji wa Kahama, Mchungaji Kusekwa aliendesha mkutano wa uinjilisti wa wiki tatu na roho 446 zilibatizwa. Wawili kati yao walikuwa makasisi wa Kanisa Katoliki, saba walikuwa maafisa wa polisi, na saba walikuwa Mashehe wa Kiislamu.

**Kiongozi Mwenye Nguvu katika Huduma ya Uchapishaji**

Mchungaji Kusekwa pia alijulikana kama kiongozi aliyefanikiwa kuongoza wainjilisti wa vitabu nchini Tanzania. Mchungaji Steve Bina anasema Mchungaji Zakayo Kusekwa alikuwa na mapenzi na kazi aliyoifanya na hakuwahi kuridhika na ubora wake. Alijua kazi yake na aliipenda na matokeo yake yalionekana. Aliacha urithi katika kazi ya uchapishaji nchini Tanzania.

Dk. Mpoki M. Ulisubisya, balozi wa Tanzania nchini Kanada, alisema, "Ninamkumbuka kama mtumishi wa Bwana aliyejitolea ambaye alikuwa na bidii sana kwa Huduma ya Uchapishaji hivi kwamba huduma hiyo ilikuwa karibu kufanana na jina lake kuu. Alikuwa mzungumzaji mzuri mwenye kuhamasisha; aliyeimba nyimbo bora zaidi kwenye Huduma ya Uchapishaji zilizokuwa na mwelekeo na usadikisho kwa Mungu aliyemtumikia."

Mwaka 1986 Tanzania General Field ilimtuma Mzee Yohana Lukwaro kwenda Zanzibar kama mwinjilisti wa vitabu. Mzee Kusekwa alidumisha mawasiliano naye mara kwa mara. Mwaka 1989 ilibidi Mzee Lukwaro arudi kutoka Zanzibar. Hivyo Mzee Ibrahim Alex Juma alitumwa kutoka Mwanza kwenda Zanzibar kuchukua nafasi yake. Mzee Juma alikutana na changamoto nyingi sana katika ardhi hii ya Waislamu, lakini Mchungaji Zakayo Kusekwa alimtia moyo avumilie na asikate tamaa. Mzee Juma alisema Mchungaji Kusekwa alipenda kuvuna roho wakati wowote, na mtu wa kwanza alibatizwa kwa siri nyakati za usiku na Mchungaji Zakayo Kusekwa.

Mchungaji Zakayo Kusekwa hakuwahi kumbagua mtu yeyote katika idara ya uinjilisti wa vitabu. Aliwapenda wote kutoka ndani ya moyo wake. Nyumba yake huko Arusha mara nyingi ilijaa wainjilisti wa vitabu waliokuja kumtembelea. Pia aliwatembelea majumbani mwao. Amina Kikula, mwinjilisti mstaafu wa vitabu, alisema wakati Mchungaji Kusekwa alipomtembelea nyumbani kwake Dar es Salaam wakati mmoja, alikula pamoja nao, jambo ambalo lilikuwa na athari ya milele kwake na kwa mume wake. Aliwapenda watu jinsi walivyokuwa. Zaidi ya uwezo wake wa kuuza vitabu, alikuwa mwandishi hodari. Aliandika vitabu kama vile: *Mwongozo Katika Matengenezo ya Afya na Ulaji wa Nyama* (*Guidance on Healthy Reformations and Meat-eating*), *Sayansi ya Kikristo katika Kuuza Vitabu* (*Christian Science on Selling Books*), *Visa Na Matendo ya Wainjilisti wa Vitabu* (*Ushuhuda na Matendo ya Wainjilisti wa Vitabu*).

**Aongoza idara ya uchapishaji**

Aliongoza idara ya uchapishaji kwa zaidi ya miaka 30: Tanzania General Field (1960-1963; 1968-1971), Majita-Ukerewe Field (1964-1965), South Nyanza Field (1972-1974), na Tanzania Union Mission (1975- 1995). Kwa sababu ya bidii yake, alipewa jina la utani la *Scania.* Alipanga mikutano na kuongoza semina nyingi ili kuwatayarisha wasambaza-injili wa vitabu kotekote nchini. Semina zake za mara kwa mara ziliundwa ili kulihamasisha na kulipa ari jeshi la wainjilisti wa vitabu. Aliwahurumia na kuwatetea wainjilisti wa vitabu na sikuzote aliwatia moyo wasonge mbele. Wainjilisti wa vitabu walikuwa na ujuzi wa kuuza na kuongoa watu, na maarifa katika Roho ya Unabii na mada nyinginezo. Moja ya mikutano iliyokumbukwa sana ni ile ya Dodoma mwaka 1976. Ilihudhuriwa na wainjilisti wa vitabu zaidi ya 600 kutoka kote nchini Tanzania na viongozi wa idara za uchapishaji kuanzia Konferensi Kuu hadi ngazi ya mtaa.

**Atakumbukwa kwa mengi**

Mchungaji Kusekwa atakumbukwa kwa uongozi wake wa maono katika uanzishwaji wa Seminari ya Huduma ya Vitabu jijini Mwanza (iliyogharimu Tsh. Milioni 34) ambayo jiwe lake la msingi liliwekwa na RL McKee, Mkurugenzi Mshiriki wa Uchapishaji wa Koferensi Kuu Oktoba 29, 1989, na kuzinduliwa mnamo Septemba 26, 1993, na Mchungaji Campos, mkurugenzi wa idara ya uchapishaji ya Konferensi Kuu. Kwa

kuwa seminari haikuendelea kama ilivyokusudiwa, Union hiyo iliuza jengo hilo kwa Konferensi ya Nyanza Kusini.

**Miaka ya Baadaye**

Mchungaji Kusekwa alistaafu rasmi Februari 28, 1996, baada ya miaka 41 ya utumishi. Mada yake ya mwisho ilikuwa kwenye Kikao cha Union ya Tanzania cha 1995. Alisimulia kisa cha maendeleo ya kanisa tangu mwanzo hadi wakati wa kustaafu kwake. Alisoma 2 Timotheo 4:7-8 , UV : “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda. Sasa nimewekewa taji ya uadilifu, ambayo Bwana, Mwamuzi mwadilifu, atanikabidhi siku ile, wala si mimi tu, bali na wale wote ambao wametazamia kufunuliwa kwake.” Alipongeza juhudi za mke wake mpendwa ambaye alikuwa katibu wake.

**Kurudi nyumbani na umauti**

Januari 1996 Mchungaji Zakayo Kusekwa Mbuti alihama kutoka Arusha kwenda Mwanza, akiishi Nundu eneo la Nyakato. Alikuwa akishughulika na shughuli mbalimbali ndani na nje ya kanisa hadi alipopumzika katika Bwana, kutokana na kuugua saratani, Julai 18, 1999. Alizikwa Julai 21, 1999 katika Viwanja vya Kanisa la Waadventista Wasabato Nyakato, jijini Mwanza. Mchungaji Joshua Kajula, mkurugenzi wa uchapishaji na katibu wa idara ya Union hiyo, aliendesha ibada ya mazishi. Alimpongeza Mchungaji Kusekwa kwa kuwa ni shujaa aliyeitetea imani yake na kujitoa katika kazi ya Mungu kwa moyo wake wote.